

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 15th July, 2026

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 10:30 a.m.*

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Next Order.

Clerk-at-the-Table: Notices of Motion

NOTICES OF MOTION

Provision of Office equipment to Lamu beach management units (BMU)

MCA Amina Hassan Bwanamkuu (Nominated): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to give a notice of the following motion:-

AWARE THAT, the Beach Management Units (BMU) within Lamu County play a critical role in the co-management of fisheries resources, record-keeping, licensing and co-ordination with the County Government and the State Department for fisheries.

FURTHER AWARE THAT, the effective execution of these functions requires adequate Office equipment, including but not limited to desks, chairs, filing, cabinets, computers/laptops and printers.

NOTING THAT, the current lack of sufficient office equipment has hindered the timely and efficient administration of BMU affairs including data collection, financial record-keeping and communication with stakeholders.

NOW THEREFORE THE ASSEMBLY RESOLVES THAT:

1. The relevant authority County Department for Fisheries and Blue Economy be to allocate funds for the provisioning of Office equipment to all registered Beach Management Units within the Lamu County.
2. A needs assessment be conducted across the BMUs to determine the specific equipment requires of each unit.
3. Priority be given to BMUs with the least capacity to ensure equitable distribution of resources.
4. A progressing report on the implementation of this motion be submitted to the Assembly within three months.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Next Order.

Clerk-at-the-Table: Statements.

STATEMENTS

Taarifa kuhusu taa za barabarani zisizofanya kazi katika eneo la Matondoni

MCA Somoe Abdulrahman Mahmoud (Nominated): Asante Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika kwa mujibu wa kanuni ya kudumu ya 47 ningependa kuomba taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa kamati ya kisekta ya barabara na uchukuzi kuhusu kutofanya kazi kwa taa za barabarani katika eneo la Matondoni.

Kwa muda mrefu sasa, wakazi wa Matondoni wamekuwa wakiishi katika giza totoro baada ya taa za barabarani kuzimika kufuatia Serikali ya Kaunti kushindwa kulipa bili za umeme kwa muda mrefu.

Kutokuwepo kwa taa hizo kumeongeza hali ya ukosefu wa usalama, kumeathiri shughuli za kiuchumi na kusababisha ugumu wa usafiri na shughuli nyingine za kijamii wakati wa usiku. Hali hii imewaathiri zaidi wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.

Kutokana na hali hiyo, naomba Mwenyekiti wa kamati husika kutoa taarifa kuhusu masuala yafuatayo:

1. Serikali ya Kaunti inadaiwa kiasi gani cha fedha kuhusiana na bili za umeme za taa za barabarani katika eneo la Matondoni.
2. Sababu zilizosababisha kuchelewa kulipwa kwa bili hizo za umeme.
3. Hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Kaunti ili kuhakikisha kuwa umeme unarejeshwa na taa hizo zinaanza kufanya kazi mara moja.
4. Mikakati ya muda mrefu ambayo Serikali ya Kaunti imeweka ili kuzuia tatizo kama hili kutokea tena katika siku zijazo.

Naiomba Serikali ya Kaunti kuchukua hatua za haraka kurejesha huduma ya taa za barabarani ili kuhakikisha usalama na ustawi wa wakazi wa Matondoni.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Response from Chair, Vice Chair or any Member of the relevant Departmental Committee.

MCA Amina Hassan Bwanamkuu (Nominated): Asante Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika kwa vile wiki ijayo tunafunga Bunge kwa ajili ya kwenda kupumzika basi nitajibidiisha niweze kuleta majibu wiki ijayo.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Mheshimiwa Somoe umeridhika na majibu yake.

MCA Somoe Abdulrahman Mahmoud (*Nominated*): Ndio nimeridhika Bwana Naibu Spika.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

MOTION

Establishment of fire hydrants and portable fire extinguishers across designated areas in Lamu County

MCA Barisa Deko Bana (*Basuba*): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I beg to move the following motion:

AWARE THAT, Section 94 of the County Governments Act 2012 and the Fourth Schedule to the Constitution place disaster management including the fire prevention and firefighting services among the functions devolved to County Governments.

NOTING WITH THE CONCERN that, Lamu County comprising densely populated informal settlements, busy market centres and expanding infrastructure around the Lamu Port (LAPSSET) corridor, remains highly vulnerable to fire outbreaks.

FURTHER NOTING that, Lamu County currently has an acute shortage of strategically located fire hydrates and readily accessible portable fire extinguisher in public buildings, markets, schools, health facilities and residential areas. Resulting in a delaying responses and liaise on distant or adequate water resources during fire emergency.

DEEPLY CONCERNED that, recent fire incident within the County including those affecting residential structures, business premises and public markets have led to loss of property largely attributable to the absence of readily available firefighting infrastructure.

***Disclaimer:** The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

RECOGNIZING that, the World Health Organization and best practice in urban fire safety planning recommend the installation of fire hydrants at intervals not exceeding designated safe distances within urban and peri-urban centres, alongside mandatory provision of portable fire extinguishers in public and commercial buildings.

NOW THEREFORE, this House resolves that the County Government of Lamu through the Department responsible for County Disaster Management Unit:

- Undertakes an immediate County-wide fire risk mapping and needs assessment to identify high-risk areas for proper fire preventions.
- Develops and implements a fire hydrant installation programme, establishing an adequate network of power/high-pressure fire hydrants connected to reliable water sources across the identified high-risk and high-density areas.
- Procures and installs portable fire extinguishers in all County-owned public buildings, markets, schools, health facilities and other public installations.
- Allocates adequate budgetary provision for the procurement, installation and routine maintenance of firefighting equipment in the County Fiscal Strategy Paper and subsequent annual budget/appropriation processes.
- Establishes a maintenance and inspection schedule to ensure all installed hydrants and extinguishers remain functional alongside regular servicing, refilling and replacement as required.

(Seconded)

Motion Proposed

Members Contributions

MCA Aisha Ali Abdulrahman (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika.

Bwana Naibu Spika nimesimama kuunga na kuchangia mada iliyoletwa na

Mheshimiwa Barisa Deko. Kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Deko kwa kuileta mada hii kwa wakati ufaao. Kusema kweli Kaunti hii yetu ya Lamu ni lazima iwe na kizima moto tukizingatia ya kwamba maafa ya moto hutoa kila mara. Kwa mfano hivi majuzi kulitokea maafa ya moto katika eneo la Mpeketoni lakini la kusikitisha hakukuwa na kizima moto. Kwa hivyo itakuwa bora kila Wadi iweze kupewa kizima moto ili iwapo mikasa hii inapotokea wananchi waweze kusaidika kwa haraka.

MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimesimama kuchangia mada iliyoletwa na Mheshimiwa Barisa Deko. Mada hii ni mada mzuri sana kwa sababu mikasa ya moto hutokea kila wakati katika Kaunti hii yetu ya Lamu. Tukiangalia katika Wadi yangu ya Mkomani hakuna barabara lakini ningeiomba Serikali ya Kaunti itafute njia mbadala ya kutafuta vifaa vya kuzimia moto ili tuweze kusaidia jamii wakati wanapofikwa na mikasa ya moto.

Bwana Naibu Spika nakumbuka nilileta hoja nyingi hapa Bungeni kuhusiana na mikasa ya moto katika Wadi yangu ya Mkomani lakini la kusikitisha sijapata usaidizi wowote isipokuwa jamii wanasaidiana wenyewe kwa wenyewe kuuzima moto wakati wa mikasa hiyo inapotokea. Mimi pia ni Mmoja wa waathirika wa mkasa wa moto lakini naishukuru jamii kwa usaidizi wao lakini la kusikitisha ni kwamba iwapo Kaunti nzima itakosa vifaa vya kuzima moto basi tunaelekea wapi? Hii ni aibu kubwa sana kwa sababu wananchi waliweza kutupigia kura ili tuweze kuwasaidia. Na mikasa hii ikitokea ni lazima sisi kama Waheshimiwa tuweze kuweka mgao wa pesa ya kuweza kununua vifaa kama hivyo.

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimesimama kuunga mkono mada iliyoletwa na Mheshimiwa kutoka Wadi ya Basuba. Kwa hakika Lamu yetu saa hii imepanuka na nina Imani miaka ijayo itakuwa sambamba na nchi ya Singapore kwa sababu tunaiona bandari yetu

imeanza kunawiri na vijana wetu wataanza kupata ajira. Na kama hatuna vifaa vya kuzimia moto basi itakuwa ni hatari kubwa sana kwa Kaunti hii yetu ya Lamu.

Pili hii mada ni muhimu sana lakini ningeiomba Serikali ya Kaunti iweze kupeana mafunzo ya namna ya kutumia vifaa hivyo kwa wafanyibiashara na wananchi kwa ujumla.

MCA James Njaaga Kariuki (Hindi): Asante sana Bwana Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii muhimu. Kwanza ningependa kuchukua nafasi hii ili niweze kumshukuru Mheshimiwa Barisa Deko kwa kuleta mswada huu hapa Bungeni. Bwana Naibu Spika katika Wadi yangu tumeweza kutokewa na mikasa mitatu ya moto. Kwa hivyo nimefurahi kuiona mada hii hapa Bungeni kwa sababu inatoa mwelekeo mzuri sana katika Kaunti hii yetu ya Lamu na ningeiomba Idara husika ichore ramani na waweze kujua ni sehemu gani wataweza kuweka vifaa hivyo ili mikasa kama hiyo ikitokea vifaa hivyo viweze kufanya kazi kwa kasi sana.

Jambo la pili Bwana Naibu Spika ningeiomba Idara husika iweke vifaa ambavyo mtu anaweza kutembea navyo popote aendapo. Pia ningewaomba wazima moto wawe na maji ya kutosha wakati wanataka kwenda kuzima moto sehemu iliyopatikana na mkasa wa moto.

MCA Mercy Riziki Nzai (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika hata mimi nimesimama kuchangia mada iliyoletwa na Mheshimiwa Barisa Deko. Langu ni kupenda kusisitiza ya kwamba tuweze kupata kituo ambacho kitaweza kuwasaidia wananchi iwapo majanga ya moto yataweza kutokea.

Mover's Response

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika ningependa kuchukua fursa hii kuweza kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu kwa kuchangia hoja niliyoleta hapa Bungeni. Iwapo tutaipitisha hoja hii basi italeta manufaa katika Kaunti hii yetu ya Lamu. Jambo lengine ni kwamba vijana wetu pamoja na wananchi kwa ujumla waweze kupewa mafunzo ya namna

ya kutumia vifaa hivyo ili majanga ya moto yanapotokea basi waweze kuzima haraka iwezekanavyo. Pia ni lazima kila Shule za mabweni ziweze kuwekwa mabomba ya maji ili majanga ya moto yatakapotokea wahusika waweze kuuzima moto huo haraka iwezekanavyo. Mwisho namalizia kwa kuiomba Ofisi yako iweze kuishughulikia kwa kina jambo hili.

(Question put and agreed upon)

ADJOURNMENT

[Deputy Speaker (Honorable Paul Njuguna Kimani)]: Honorable Members, there being no any other business, the Assembly stands adjourned until today Wednesday 15th July 2026 at 2:30pm.

The Assembly rose at 11:30am.